

# Magaidi wauo 11

Uhuru

## Msumbiji

15  
1  
88

p. 2

MAPUTO, Msumbiji

MAGAIIDI wa MNR nchini Msumbiji walishambulia mji wa Manhica uliopo umbali wa kilomita 80 kaskazini mwa mji wa Maputo ambako waliua raia 11 na kujeruhi vibaya wengine 28 hapo juzi Jumatano.

Habari zilizotolewa na gazeti moja nchini humo, zimesema kwamba askari waliokuwepo katika mji huo walifanikiwa kuwaua magaidi wanane jana. Magaidi hao walishambulia duka na ghala la shirika la reli ya nchi hiyo na kuwasha moto magari matatu na kuharibu kitengo cha kutengeneza madawa.

Pia imeelezwa kuwa mtoto wa miaka 12 ambaye alikuwa ametekwa na magaidi wa MNR alitekwa na askari wa serikali akiwa anapigania magaidi wakati wa mapambano hayo.

Mtoto huyo ambaye ni mvulana alisema alipokuwa akiishi na magaidi hao aliamriwa kuwaua wanawake kumi baada ya kunywa vidonge ambavyo vinadaiwa vinaongeza ari na ujasiri.

Magaidi wa MNR ambao wamekuwa wakipambana kwa muda wa miaka 12 kuangusha serikali halali ya Msumbiji hivi karibuni yamezidisha harakati zake kwa kushambulia makazi ya raia na magari.